



KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO
KONFERENSI YA KASKAZINI MASHARIKI MWA TANZANIA

CHANGIZO LA UJENZI WA OFISI ZA
KONFERENSI

17 Desemba 2023





TAMKO LA UTUMEWA KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO

UTUME WETU (OUR MISSION)- Utume wa kanisa la Waadventista wa Sabato ni kuwaita watu wote wawe wanafunzi wa Yesu, Kutangaza Injili ya milele katika muktadha wa ujumbe wa malaika wa tatu wa Ufunuo 14:6-12, na kuandaa ulimwengu marejeo ya Kristo yaliyo karibu.

UTEKELEZAJI WA UTUME WETU WETU (OUR METHOD) - Kwa kuongozwa na Biblia na Roho Mtakatifu, Waadventista wa Sabato hutekeleza utume huu kupitia maisha yanayoakisi alivyoishi Kristo, katika kuwasiliana, kufanya wanafunzi, kufundisha, kuponya, na kuhudumia.

NJOZI YA UTUME WETU (OUR VISION) - Kwa kupatana na Mafunuo ya Biblia, Waadventista wa Sabato tunauona utume wetu ukifikia kilele katika mpango wa Mungu wa urejeshwaji wa viumbe vyake katika ukamilifu wa mapenzi yake na haki yake.



TAARIFA YA MRADI WA UJENZI WA JIMBO LA NETC

Mradi huu ulianza Mnamo mwaka 2021, kwa hatua mbalimbali, ambapo Hatua ya Kwanza ilianza kwa Kusafisha eneo, kuchimba msingi, kuweka Nondo za Msingi na kumimina Jamvi kwaajili ya Msingi. Hatua ya pili ni Kupandisha Nguzo za chini Zaidi ya 95 na hatua ya tatu ni kuweka mirunda, kusuka Nondo, kufunga Mfumo wa Umeme na kumimina jamvi kwaajili ya ghorofa ya kwanza nah atua zote zimekamilika.

Zaidi ya Shilingi 421,307,000 zilikusanywa kwaajili ya mradi huo kutoka kwenye Makanisa Mahalia na Wadau wa Maendeleo.

Tangu Mradi huu ulipoanza hadi kufikia sasa zimetumika Tsh. MILION 416,484,000.

Katika Changizo hili la kuchangia Zaidi ya shilingi million 685 ni kwaajili ya kuendeleza Mradi huu kwa Kukamilisha eneo la Chini la Jengo, kupandisha Nguzo za Ghorofa ya Kwanza na Kupaua.



HATUA ZA UJENZI



Zoezi la kuchimba msingi wa jengo



Muonekano wa juu wa msingi wa jengo



HATUA ZA UJENZI



Muonekano wa Nguzo za kushikilia ghorofa ya kwanza



Zoezi la kusuka nondo kwenye formwork



HATUA ZA UJENZI



Zoezi la Kumimina Jamvi



Picha ya Juu ya jengo baada ya hatua ya kumimina jamvi Kukamilika



RATIBA

MUDA	TUKIO	MHUSIKA
02:00-02:30	KUWASILI	Wote
02:30-03:00	UIMBAJI SEHEMU YA 1	<ol style="list-style-type: none">1. Kwaya ya Kandoto vijana2. Kwaya ya Sangu3. Kwaya ya Chemchem4. kwaya ya Kísima5. kwaya ya Same6. Kwaya ya Mnazi Mmoja
03:00-03:30	ZIARA YA ENEO LA OFISI	S. William (Estate Manager)/ Wageni wote waalikwa
03:30-03:50	PROGRAM MAALUMU	Watafuta Njia Mkonga na Same
03:50-04:00	UIMBAJI AWAMU YA 2	<ol style="list-style-type: none">1. Kwaya ya Kana2. kwaya ya Mji Mpya (Korogwe)3. Kwaya ya Karmel Vijana
04:00-04:20	UKARIBISHO WA MGENI RASMI	Watafuta Njia Mkonga
04:20-04:30	UKARIBISHO NA UTAMBULISHO	Pr. E. Kajiru (Katibu Mkuu NETC)
04:30-04:35	WIMBO WA KWAYA	Kwaya ya Njoro Family
04:35-05:00	NENO LA MUNGU NA MAOMBI	Pr, Prof, P. Manu (Vice Chancellor University of Arusha)
05:00-05:05	WIMBO WA KWAYA	Kwaya ya Kana
05:05-05:20	PROGRAM MAALUMU	Watafuta njia Mkonga
05:20-05:30	RISALA	S. William (Estate manager NETC)
05:30-05:35	WIMBO WA KWAYA	Kwaya ya Mji mpya (Korogwe)
05:35-05:45	SALAMU ZA MKUU WA WILAYA	Mhe. Kasilda Mgeni (Mkuu wa wilaya ya Same)
05:45-06:00	UKARIBISHO MAALUMU WA MGENI RASMI	Pr. M. Nzumbi (Askofu wa Jimbo NETC)
06:00-07:10	HOTUBA YA MGENI RASMI NA CHANGIZO	Mhe. Nurdin Hassan Babu (Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro)
07:10-07:20	WIMBO WA KWAYA	Kwaya ya Kandoto Vijana
07:20-07:30	TAARIFA YA CHANGIZO	Eld. J. Singo (Assistant Treasure NETC)
07:30-07:40	SALAMU ZA SHUKRANI	Eld. E. Kakore (Mwenyekiti kamati ya Ujenzi)
07:40-07:50	SHUKRANI NA ZAWADI	Eld. E. Kisimbo (Mhazini wa Jimbo NETC)
07:50-08:00	OMBI LA BARAKA	Pr. E. Ijiko (Askofu mstaafu jimbo la NETC)
08:00 --	CHAKULA	Wote



WIMBO MKUU

NO. 03

Mungu Atukuzwe

1

Mungu atukuzwe, kwa mambo
maku, Upendo wake ulitupa Yesu,
Aliyejitoa maisha yake, tuwe nao
Uzima wa milele.

Chorus:

*Msifu, msifu, dunia sikia,
Msifu msifu watu wafurahi,
Na uje kwa Baba kwa Yesu Mwana,
Ukamtukuze kwa mambo yote*

2

Wokovu kamili, zawadi kwetu,
Ahadi ya Mungu kwa Ulimwengu,
Wanaomwamini na kuungama,
Mara moja wale husamehewa.

3

Alitufundisha mambo makuu,
Alihakikisha wokovu wetu,
Lakini zaidi ajabu kubwa,
Yesu atakuja na tutamwona.